# MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO HALMASHAURI YA MJI KIBAHA KWA MWAKA 2022/2023 - 2024/2025

## SURA YA KWANZA

## 1.0. UTANGULIZI

***Mheshimiwa Mwenyekiti;*** Halmashauri ya Mji Kibaha katika kipindi cha mwaka 2022/2023 imepanga kutekeleza majukumu yake ya kimsingi yenye lengo la kutoa huduma bora na kuondoa umaskini kwa Wananchi wake. Malengo haya yameainishwa katika Mpango mkakati (Strategic Plan) wa Halmashauri wa mwaka 2021/2022 - 2025/2026, Ilani ya uchaguzi mkuu 2020-2025, Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati alipolihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021, Sheria ya bajeti, SURA 439 pamoja na kanuni zake, Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu Tatu, Ushirikiano wa Kimaendeleo (DCF), Sanjari na makubaliano mengine ya kikanda na Kimataifa ambayo Serikali imeyaridhia. Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's), Sera mbalimbali za Kisekta zikiwepo za viwanda na uwekezaji pamoja na Miongozo mbalimbali kutoka serikali kuu.

## 1.1 Dira, Dhamira na Malengo ya Halmashauri

### 1.1.1 Dira (Vision)

'Dira ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha ni "*kuwa halmashauri yenye mazingira mazuri na huduma za ubora wa juu kwa maendeleo endelevu ifikapo 2025*"

### 1.1.2 Dhamira (Mission)

"Dhamira ya Halmashauri ya mji wa Kibaha "*Kutoa huduma zenye ubora wa hali ya juu na kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya kuwekeza kwa matumizi mazuri ya rasilimali zilizopo kwa maendeleo endelevu*"

### 1.1.3 Malengo (Objectives)

A. Kuboresha huduma na kupunguza maambukizi ya UKIMWI.
B. Uboreshaji, uendelezaji na utekelezaji kikamilifu mpango wa Taifa wa kupambana na rushwa.

C. Kuboresha upatikanaji wa huduma bora za kijamii.
D. Kuongeza ubora wa huduma za kijamii na miundombinu.
E. Kuwezesha huduma za kiutawala na kukuza utawala bora.
F. Kuboresha ustawi wa jamii, jinsia na kuiwezesha jamii.
G. Kukuza huduma za dharura na usimamizi wa maafa na majanga.
H. Kuendeleza na kusimamia maliasili na usafi wa mazingira.

### 1.2 Wadau wa Halmashauri ya Mji Kibaha na matarajio yao

Halmashauri ya Mji Kibaha inalo jukumu kubwa la msingi la kutoa huduma za kiuchumi na kijamii kwa wakazi wake. Ili kutekeleza jukumu hilo, Halmashauri inashirikiana na wadau mbalimbali ambao hutoa mchango wao ili kuboresha huduma zinazotolewa kwa wakazi wa Mji. Wadau hao ni pamoja na waheshimiwa madiwani wa Mji Kibaha, Watumishi wa Halmashauri ya Mji Kibaha, Serikali Kuu, Wafadhili mbalimbali, Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs/CBOs), Sekta binafsi, Vyama vya Ushirika na Jamii.

### 1.3 Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo

Halmashauri ya Mji Kibaha inao uwezo na fursa mbalimbali ambazo zikitumika vizuri zitasaidia kuinua kiwango cha maisha ya wakazi wake. Uchambuzi wa hali halisi umebainisha kuwepo kwa fursa na vikwazo vifuatavyo:

#### 1.3.1 Fursa

i. Mtandao mzuri wa mawasiliano ya barabara na makampuni ya simu.
ii. Nguvu kazi ya kutosha kuweza kufanya kazi za maendeleo.
iii. Uongozi unaozingatia kanuni, sheria, uwazi na uwajibikaji.
iv. Ardhi ya kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa uwekezaji na makazi.
v. Kuwepo kwa makampuni, taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO's) ambayo yanasaidia kutoa huduma kwa wananchi.
vi. Mahusiano mazuri na wadau wanaochangia maendeleo ya wakazi kwa ujumla wake.
vii. Kuwepo kwa eneo kubwa linalofaa kwa uwekezaji wa ndani na nje.

### 1.3.2 Vikwazo

Pamoja na uwezo na fursa zilizopo kwenye Halmashauri ya Mji Kibaha, bado kiwango cha kufikia malengo yanayowekwa si cha kuridhisha kutokana na changamoto na vikwazo vifuatavyo:

i. Ongezeko la idadi ya watu wanao hamia kutoka Jiji la Dar es salaam na maeneo mengine inachangia upungufu wa huduma kama vile Afya na maji.
ii. Ufinyu wa rasilimali fedha za kutosheleza mahitaji ya Jamii
iii. Kuenea kwa ugonjwa wa UKIMWI.
iv. Kupanda kwa gharama za bei za huduma kwa wakazi.
v. Mwamko Mdogo wa wananchi kuchangia shughuli za maendeleo
vi. Fedha za miradi ya maendeleo kuchelewa kutolewa na wakati mwingine kutotolewa kabisa.
vii. Baadhi ya wananchi kutokuwa tayari kulipa Kodi na wengine kutoa takwimu zisizo za ukweli hivyo kupelekea kupoteza mapato ya Halmashauri
viii. Kutokamilika kwa miradi ya maji kwa wakati Kutokana na kukosa Fedha.
ix. Kuchukuliwa kwa baadhi ya vyanzo vikuu vya mapato ya ndani kama vile Kodi ya majengo na ushuru wa mabango kumechangia kupungua kwa makusanyo ya mapato ya ndani

### 1.3.3 Mikakati ya kukabiliana na vikwazo

- Kuongeza juhudi katika ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.
- Kuendelea kupanga na kupima viwanja katika Halmashauri ya mji kibaha ili kurahisisha utoaji wa huduma za Afya, Maji na Elimu.
- Kuendelea kuhamasisha wananchi kujitokeza kuchangia shughuli za maendeleo.
- Halmashauri inawaelekeza wananchi wakulima na wafugaji kuwa na kilimo/ufugaji wa kisasa.
- Kuwaelimisha wananchi ulipaji wa Kodi za serikali kwa wakati na kuwapatia motisha walipakodi wasio wasumbufu ili kuwavutia wale wasiolipa.
- Kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani
- Kurasimisha biashara zisizo rasmi na kuhakiakisha zinachangia kodi
- Kuendelea kuandaa mazingira mazuri kwa ajili ya kuvutia wawekezaji.

## 1.4 Vipaumbele vya Halmashauri kwa mwaka 2022/2023

### 1.4.1 Elimu

- Kuboresha utoaji huduma ya Elimu ya Msingi na Sekondari katika ngazi zote kwa kuongeza upatikanaji wa vitabu, vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, mabweni, bwalo la chakula, majengo ya utawala na madawati.

### 1.4.2 Kilimo

- Kuongeza uwezo wa uzalishaji wa mazao bora ya kilimo kwa kufuata mnyororo wa thamani na matumizi mazuri ya pembejeo na zana za kilimo.
- Kuboresha huduma za ugani kwa kutoa mafunzo kwa maafisa ugani.

### 1.4.3 Mifugo na uvuvi

- Kuongeza uwezo wa uzalishaji wa mazao ya mifugo na uvuvi.
- Kuainisha na kuboresha shughuli za mifugo na uvuvi kwa kutoa vitendea kazi.
- Kuboresha mazingira na shughuli za mifugo kwa kuwapatia mafunzo watalaam na wafugaji.
- Kuboresha huduma za kinga na tiba kwa mifugo kwa kujenga/kukarabati miundombinu na kutoa nyezo za kutolea huduma za afya kwa mifugo katika ngazi zote.

### 1.4.4 Majengo

- Kuboresha pamoja na kusimamia ujenzi/ ukarabati wa majengo yaliyopo na yanayoendelea kujengwa.

### 1.4.5 Afya

- Kuboresha huduma za kinga na tiba kwa kujenga/kukarabati miundombinu na kutoa nyenzo za kutolea huduma za afya katika ngazi zote.
- Kutoa mafunzo kwa wataalam wa afya.

### 1.4.6 Ardhi na Maliasili

- Kuboresha matumizi ya maliasili.
- Kuboresha makazi kwa kupima na kuendeleza viwanja

### 1.4.7 Fedha na biashara

- Kubuni na kuimarisha vyanzo vya  Mapato  vya Halmashauri.
- Kuboresha mapato ya Halmashauri kwa kutumia mfumo wa kielektroniki
- Kuendelea kuhuisha takwimu za vyanzo vya mapato

### 1.4.8 Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji

- Kusimamia maandiko ya miradi na kutafuta wawekezaji
- Kuhuisha wasifu wa kiuchumi na Kijamii (Socio – economic profile) wa Halmashauri ya Mji Kibaha na Wasifu wa uwekezaji (Investment Profile)
- Kufanya mapitio na kuhuisha takwimu za Halmashauri ya Mji Kibaha.
- Kufanya ufuatiliaji na tathimini ya miradi ya Halmashauri (M & E).

### 1.4.9 Raslimali watu na Utawala

- Kuimarisha programu ya mafunzo kwa Watumishi na Madiwani.
- Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji
- Kuboresha mazingira ya ofisi za kufanyia kazi.

### 1.4.10 Maeneo ya mtambuka

- Kuzuia maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI.
- Kuboresha asasi zilizo katika mapambano ya virusi vya UKIMWI.
- Kuimarisha masuala ya usafi na uboreshaji wa Mazingira.
- Kuimarisha huduma za dawati la jinsia.
- Kupiga vita na kuzuia suala la Rushwa katika Halmashauri.
- Kuwezesha makundi maalum yakiwemo vikundi vya wananwake, vijana, wazee na walemavu.

## 1.5 Sera na Miongozo Iliyozingatiwa Katika Bajeti ya 2022/2023

Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025 umeandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa uandaaji wa Bajeti kutoka Serikali Kuu (umetolewa mwezi Novemba, 2021), Sheria ya Bajeti SURA 439, Sera na Malengo yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-20/25, Dira ya maendeleo ya Taifa – 2025 na Maelekezo ya Serikali yaliyoainishwa na Mheshimiwa Rais alipolihutubia Bunge tarehe 22 Aprili, 2021, Malengo ya maendeleo Endelevu (SDGs), Mwongozo wa Ushirikiano wa Maenedeleo, na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Serikali imeyaridhia

**A. Maelekezo ya Jumla yaliyotolewa katika Mwongozo 2020/2021 kwa Serikali za Mitaa wakati wa kuandaa bajeti.**

Katika maandalizi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2022/2023, maelekezo yafuatayo yamezingatiwa:

i. Kusimamia na kudumisha masuala ya ulinzi na usalama;
ii. Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika maeneo ya utawala kwa
iii. kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa,
iv. Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili wa Wanawake na Watoto na kuwezesha kufanyika kwa vikao vya kisheria vya Kamati za Maendeleo za Kata na mikutano ya Vijiji, Mitaa na Vitongoji;
v. Kupitia, kurekebisha na kutunga Sheria Ndogo ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato na Utawala Bora;
vi. Kutumia Mpango Mkakati wa Halmashauri uliohuishwa, Mwongozo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo Ulioboreshwa mwaka 2019, Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 katika kuainisha vipaumbele vya maendeleo na kujumuishwa kwenye Mpango na Bajeti ya Halmashauri;
vii. Kutumia mifumo ya TEHAMA ikiwemo mifumo ya ukusanyaji wa mapato na matumizi, Mipango na Bajeti, utoaji na uwekaji wa taarifa za Umma katika Tovuti za Halmashauri;
viii. Kuhakikisha Kamati za Bajeti zinaandaa na kusimamia mpango na bajeti, ugawaji wa rasilimali fedha zinazopokelewa kila mwezi na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kila robo mwaka kwa Sekretarieti za Mikoa kwa mujibu wa Kifungu 18(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439. Aidha, muhtasari wa kikao cha mgao wa kila mwezi uwasilishwe HAZINA na nakala OR – TAMISEMI na utakuwa ni kigezo cha kutengewa fedha kwa mwezi unaofuata;
ix. Kuandaa mipango na makadirio ya mapato na matumizi ya vituo vya kutolea huduma kama shule, vituo vya afya, zahanati, hospitali na Vijiji/Mitaa na kuijumuisha kwenye Mpango na Bajeti ya Halmashauri;
x. Kutenga fedha za ujenzi, ukamilishaji, ukarabati na ununuzi wa samani kwa ajili ya majengo ya utawala na nyumba za viongozi wa Halmashauri, Ofisi za Kata na Vijiji/Mitaa;
xi. Kutenga fedha kutoka makusanyo ya mapato ya ndani ikiwa ni sehemu ya fedha za miradi ya maendeleo kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
xii. Kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa viuadudu ili kutokomeza mazalia ya mbu;

xiii. Kutenga bajeti kwa ajili ya kutatua migogoro, kutambua maeneo ya mipaka na kuweka alama za mipaka ya Halmashauri, Kata, Vijiji/Mitaa na Vitongoji pamoja na maeneo ya hifadhi;

xiv. Kutenga kiasi kisichopungua shilingi 200,000 kila robo mwaka kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi kwa kila Kijiji/Mtaa. Aidha, kwa Halmashauri zinazokusanya mapato chini ya shilingi bilioni moja zinaelekezwa kutenga kiasi cha shilingi 100,000 kwa kila robo mwaka kwa Kijiji/Mtaa;

xv. Kuendelea kutenga na kuweka fedha kwenye akaunti ya mikopo kwa ajili ya vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu na kufungua akaunti kwa ajili ya marejesho ya mikopo hiyo pamoja na kutoa taarifa za utekelezaji;

xvi. Kutenga fedha za ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa mujibu wa marekebisho ya kanuni za utoaji na usimamizi wa Mikopo ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2021;

xvii. Kutenga fedha kwa ajili ya marejesho ya mikopo na michango ya wanachama kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na ALAT;

xviii. Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi kwa vikundi vya Watu Wenye Ulemavu, Vijana na Wanawake;

xix. Kubuni na kuandaa maandiko ya miradi kwa kutumia Mwongozo wa Uandaaji wa Miradi ya Kimkakati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (2021) ikiwa ni pamoja na miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi;

xx. Kutekeleza Mwongozo wa OR -TAMISEMI wa utoaji wa vibali vya ujenzi na usimamizi wa ujenzi wa majengo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa uliotolewa Machi, 2018;

xxi. Kuwezesha mazingira rafiki ya kibiashara kwa kuzingatia Mkakati wa Kuboresha Mazingira Wezeshi ya Biashara Nchini wa Mwaka 2018;

xxii. Kuendelea kuboresha huduma ndogo za fedha kwa kuimarisha Kamati za Usimamizi katika usajili, kujenga uwezo wa vikundi vya fedha vya kijamii pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini;

xxiii. Kutenga maeneo na kuweka miundombinu wezeshi kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo (Wamachinga) na kuwapatia elimu ya biashara na

ujasiriamali na kuwaunganisha na taasisi za fedha na masoko ili kukuza fursa za ajira na uchumi wa maeneo husika;

xxiv. Kuimarisha mifumo ya uratibu, utekelezaji na usimamizi wa maafa ikiwa ni pamoja na usimamizi wa utekelezaji wa Muundo wa Usimamizi wa Maafa;

xxv. kuzijengea uwezo na kuhakikisha Kamati za Maafa katika ngazi zote za Serikali zinaandaa na kusimamia utekelezaji wa mipango na mikakati ya kukabiliana na maafa kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya Mwaka 2004, Mwongozo wa Taifa wa Menejimenti ya Maafa 2014 na Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2015;

xxvi. Kuwasilisha kwa Katibu Tawala wa Mkoa ahadi za fedha na miradi inayopendekezwa kutekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO's);

xxvii. Kutenga bajeti kwa ajili ya urasimishaji wa ardhi, makazi na biashara na kutoa taarifa ya utekelezaji kila robo mwaka;

xxviii. Kuzingatia Kifungu cha 41 cha Sheria ya Bajeti Sura 439, taratibu na miongozo wakati wa kuomba kibali cha kubadili matumizi ya fedha endapo mradi umekamilika na fedha zimebaki katika mradi huo au kuna sababu za kubadili matumizi ya fedha za mradi huo ili kutekeleza mradi mwingine wenye tija zaidi. Aidha, maombi hayo yawasilishwe kwa Katibu Tawala wa Mkoa kwa ajili ya kuomba kibali kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na kutoa taarifa OR-TAMISEMI. Vilevile, kubadili eneo la utekelezaji wa mradi maombi yawasilishwe kwa Katibu Mkuu OR-TAMISEMI kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa;

xxix. Kuhakikisha taarifa za mapato na matumizi yote ikijumuisha fedha zinazopokelewa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na fedha za mapato ya ndani zinazotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinabandikwa kwenye ubao wa matangazo na kuchapishwa katika tovuti husika;

xxx. Kutoa kipaumbele katika uzingatiaji wa masuala ya uchumi wa buluu na uchumi wa kidigitali katika bajeti kwa sekta husika; na

xxxi. Kuhakikisha miradi inayoanzishwa na wananchi inapatiwa ushauri wa kitaalamu kabla ya kuanza kutekelezwa.

B. **Maelekezo Mahsusi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Sekta za Afya, Elimu, Kilimo, Ardhi na Mazingira**

i. Kuboresha huduma za afya na lishe katika ngazi ya jamii na vituo vya huduma za afya kwa kutenga bajeti ya uratibu, usimamizi na kujenga uwezo kuhusu masuala ya lishe ikiwa ni pamoja na kutenga shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano kwa ajili ya huduma za lishe;

ii. Kuboresha huduma za afya kwa kujenga, kukamilisha na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya na kuviwekea vifaa na vifaa tiba na dawa; kuimarisha Bodi za afya za Halmashauri, Timu ya Uendeshaji wa Shughuli za Afya ngazi ya Wilaya, kamati za vituo vya afya, zahanati na huduma za rufaa; huduma za mama na mtoto ikiwemo huduma za chanjo; kudhibiti magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza, huduma za tiba asili na tiba mbadala; na kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya afya (NHIF), Mfuko wa Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF) na mifuko mingine inayotoa huduma za bima na Afya;

iii. Kuwatambua, kuwasajili na kuwatengamanisha na huduma watoto walio katika mazingira hatarishi wakiwemo wanaoishi na kufanya kazi mitaani, wazee na watu wenye mahitaji maalum na kuimarisha mfumo jumuishi wa usimamizi wa mashauri ya watoto walio katika mazingira hatarishi;

iv. Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kupitia OR-TAMISEMI takwimu zenye uhalisia za Elimu kulingana na Mahitaji ya bajeti zikijumuisha idadi ya Wanafunzi walioandikishwa kuingia Elimumsingi, idadi ya Wanafunzi; Shule za awali, Msingi, Sekondari, Shule za bweni, Maafisa Elimu Kata pamoja na shule mpya zinazostahili kupatiwa vibali vya usajili ifikapo tarehe 30 Januari, 2022 ili kuwezesha utengaji wa bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa Elimumsingi bila Malipo;

v. Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za msingi na sekondari kwa kujenga, kukamilisha na kukarabati miundombinu ya shule; kuwezesha michezo shuleni; kuwapatia nyenzo na vifaa wanafunzi wenye mahitaji maalum; kuimarisha masuala ya malezi na makuzi, unasihi, usalama wa mtoto, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni na nyumbani na kuandaa mikakati ya kushirikisha jamii katika kuhakikisha upatikanaji wa chakula shuleni;

vi. Kutambua na kuendeleza bunifu katika teknolojia kwa ajili ya kuziendeleza na kuboresha huduma;

vii. Kuwawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo kupata utaalam na mbinu bora kutoka kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wakubwa ambao wapo kwenye maeneo yao ili kukuza uwezo na kuendeleza kilimo cha kisasa, chenye tija na cha kibiashara;

viii. Kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Kilimo ngazi ya Halmashauri (DADPs);

ix. Kuwawezesha Maafisa Ugani kutoa huduma bora za ugani na kudhibiti ubora wa pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kushirikiana na mamlaka za utafiti na udhibiti;

x. Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda;

xi. Kutenga asilimia 20 ya mapato yatokanayo na tozo ya mazao ya kilimo (crop cess) kwa ajili ya shughuli za kilimo ikiwemo kuendeleza uzalishaji wa mazao ya kimkakati;

xii. Kutenga asilimia 15 ya mapato yatokanayo na mazao ya mifugo kwa ajili ya shughuli za kuendeleza ufugaji kwa mujibu wa Waraka wa Rais Na. 01 wa mwaka 2002 kuhusu Hatua za Kuchukua Kuzuia Kuenea kwa Magonjwa ya Mifugo Nchini;

xiii. Kutenga asilimia 5 ya mapato yatokanayo na mazao ya uvuvi kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uvuvi kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009;

xiv. Kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya Ushirika pamoja na kuweka mifumo itakayoongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wanaushirika;

xv. Kuendeleza mipango miji na matumizi bora ya ardhi kwa kuandaa mipango kabambe (master plan) ya miji ili kuwa na miji iliyopangika hususan miji midogo inayochipukia na kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Sura 113 na kutekeleza Mwongozo wa Kitaifa wa Uhamasishaji Jamii Ujenzi wa Nyumba Bora wa Mwaka 2019;

xvi. Kuendeleza na kuhamasisha matumizi bora ya ardhi kwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji ili kuwa na vijiji vilivyopangika na kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya

Vijiji, Sura 114 na kutekeleza Mwongozo wa Kitaifa wa Uhamasishaji Jamii Ujenzi wa Nyumba Bora wa Mwaka 2019;

xvii. Kuboresha shughuli za usimamizi wa mazingira kwa kuimarisha kamati za mazingira katika ngazi za Halmashauri, Kata, Mtaa/Kijiji na kuhakikisha teknolojia za uzalishaji zinazingatia uhifadhi wa mazingira; uzoaji na uondoshaji wa taka; na kuendelea kuzingatia kanuni za udhibiti wa matumizi ya mifuko ya plastiki kwa mujibu wa zuio lililotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais Mwaka 2019;

xviii. Kutenga fedha kwa ajili ya kuhifadhi maeneo oevu, vyanzo vya maji, upandaji miti, utunzaji misitu na maeneo ya hifadhi; na

xix. Kutafsiri sheria, sera, kanuni na miongozo ya Serikali katika kuratibu na kushiriki katika utekelezaji wa miradi na shughuli za hifadhi ya mazingira zinazotekelezwa na wadau mbalimbali zikiwemo asasi za kiraia, sekta binafsi na jamii zilizopo katika maeneo yao.

### 1.5. Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji

Ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti utazingatia Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa mwaka 2015 na miongozo mingine iliyopo kwenye sekta mbalimbali.

#### 1.5.1. Ufuatiliaji na Tathmini

Katika kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

i. Kuandaa Mpango Kazi shirikishi wa ufuatiliaji na tathmini wa miradi ya maendeleo ili kuendana na matakwa ya Mpango Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26);

ii. Kutenga fedha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

iii. Kuandaa viashiria vya kupima utekelezaji wa malengo ya Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili viwe vipimio vya mafanikio ya taasisi husika;

iv. Kuweka mifumo thabiti ya ufuatiliaji na tathmini na kuhakikisha kuwa malengo, shabaha na viashiria vya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) vinatafsiriwa vema katika Mpango na Bajeti;

v. Kujenga uwezo wa watumishi katika vitengo vya ufuatiliaji na tathmini na kuandaa mpango wa kurithisha watumishi wapya maarifa ili kuwa na mfumo wa ufuatiliaji endelevu;

vi. Kuendelea kutumia taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kuboresha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mpango na bajeti;

vii. Kujenga uwezo wa wakaguzi wa ndani kufanya ukaguzi kupitia mifumo ya

viii. kielektroniki (system-based auditing) ili kuongeza ufanisi;

ix. Kutoa kipaumbele na kutenga fedha kwa ajili ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa sera hususan zilizotekelezwa kwa zaidi ya miaka mitano;

x. Kuhakikisha taarifa za ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya maendeleo zinaandaliwa na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (National Projects Management Information System - NPMIS); na

xi. Kufanya vikao vya Kamati ya Bajeti kwa ajili ya kupitia na kujadili taarifa za ufualiliaji, tathmini na utekelezaji kila robo mwaka kwa ajili ya kuleta uwazi na uwajibikaji.

### 1.6 Mbinu Iliyotumika Katika Kuandaa Mpango na Bajeti.

Katika kuimarisha utawala bora na Uwajibikaji katika ngazi zote za utendaji, mpango wa mwaka 2022/2023 umeandaliwa kwa kuishirikisha jamii katika kuibua vipaumbele kwa kutumia mbinu shirikishi ya fursa na vikwazo kwa maendeleo **(O & OD)** ambapo wananchi kwa kushirikiana na watalaam katika ngazi za Mitaa na Kata wameibua Mipango yao ya maendeleo. Mipango hiyo imejadiliwa na kupitishwa

katika kamati za Maendeleo za Kata na hatimaye kuwasilishwa katika ngazi ya Halmashauri.

SURA YA PILI

## 2.0 MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI KUANZIA MWEZI JULAI, 2021 HADI DISEMBA, 2021

### 2.1 Mapitio ya Mapato

**Makadirio ya mapato 2021/2022.** Katika bajeti ya mwaka 2021/2022 Halmashauri ililenga kukusanya jumla ya Tsh. **38,952,626,768.12** kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Kati ya fedha hizo Mapato ya ndani ni Tsh. **4,561,367,650,** Mapato ya Ruzuku ya Mishahara Tsh. **22,237,022,000,** Ruzuku ya Matumizi mengineyo (OC) Tsh. **1,177,411,380.00,** Ruzuku ya Maendeleo Tsh. **5,201,035,000** na mapato toka kwa wafadhili na wadau mbalimbali Tsh. **5,912,307,010**

Aidha kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Mji Kibaha ilipokea fedha nje ya Bajeti kiasi cha shilingi **2,858,000,000,262.12** na kupelekea Bajeti kufikia kiasi cha shilingi **40,918,043,040.42** sawa na asilimia 7.5 ya ongezeko la Bajeti ya mwaka 2021/2022.

Jedwali 2.1: Mapitio ya Makisio ya Mapato Halisi ya Halmashauri kwa Kipindi cha 2021/2022 (Julai - Disemba, 2021)

| Na. | Chanzo cha Mapato | Makisio 2021/2022 | Mapato Julai – Disemba, 2021 | Mapato Halisi (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Ndani | 4,561,367,650 | 3,151,896,148.39 | 70 |
| | **Jumla Mapato ya Ndani** | **4,561,367,650** | **3,151,896,148.39** | **70** |
| **Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida** | | | | |
| 2 | Mishahara | 22,237,022,000 | 12,566,935,240 | 57 |
| 3 | Matumizi Mengineyo (OC) | 1,177,411,380.00 | 1,245,196,119.49 | 106 |
| **Jumla ya Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida** | | **23,414,433,380** | **13,812,131,359** | **59** |
| **Miradi ya Maendeleo** | | | | |
| 4 | Ujenzi wa soko la kisasa | 2,000,000,000 | 489,803,903.92 | 24 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | (Mradi Mkakati) | | | |
| 5 | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya | 800,000,000 | 0 | 0 |
| 6 | Ujenzi wa Jengo la ofisi ya Halmashauri | 1,000,000,000.00 | 174,732,853.69 | 17 |
| 7 | Mfuko wa Jimbo | 36,325,000 | 36,325,000 | 100 |
| 8 | Ujenzi wa shule ya Sekondari | 1,075,200,000 | 470,000,000 | 44 |
| 9 | Ujenzi wa miundombinu ya elimu Sekondari | 112,500,000 | 112,500,000 | 100 |
| 10 | Uboreshaji wa Elimu (LANES) | 64,510,000 | 0 | 0 |
| 11 | Umaliziaji wa Maboma ya madarasa Elimu Msingi | 112,500,000 | 0 | 0 |
| **Jumla Miradi ya Maendeleo** | | **5,201,035,000** | **1,283,361,757.61** | **25** |
| **Wadau wengine wa Mendeleo** | | | | |
| 12 | Michango ya Jamii | 100,000,000.00 | 52,342,800 | 52 |
| 13 | Elimu Bure Msingi | 634,125,620 | 192,268,478.98 | 30 |
| 14 | Elimu Bure Sekondari | 1,447,576,380 | 450,101,125.86 | 31 |
| 15 | Ada ya shule Msingi | 135,900,000 | 29,021,015.00 | 21 |
| 16 | TIKA/ CHF | 14,000,000 | 25,127,157.17 | 179 |
| 17 | NHIF | 101,909,250 | 45,198,150.00 | 44 |
| 18 | Kuchangia Papo kwa papo (User Fee) | 142,546,400 | 79,522,026.30 | 56 |
| 19 | Mfuko wa Pamoja Sekta ya Afya | 251,346,000 | 49,305,868.26 | 20 |
| 20 | Afya-RBF | 329,336,983 | 23,531,868.34 | 7.1 |
| 21 | Ruzuku ya Afya-THPS | 21,000,000 | 0 | 0 |
| 22 | Vifaa tiba (MSD) | 283,119,724 | 0 | 0 |
| 25 | TASAF - PSSN | 574,435,000 | 302,743,324.28 | 53 |
| 26 | UNICEF | 10,000,000 | 0 | 0 |
| 27 | Global Fund | 35,062,000 | 0 | 0 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 28 | Elimu-P4R Msingi | 346,581,500 | 0 | 0 |
| 29 | Elimu-P4R Sekondari | 346,581,500 | 0 | 0 |
| 30 | Usafi wa mazingira - SWASH | 24,000,000 | 0 | 0 |
| 31 | NTD | 15,549,000 | 0 | 0 |
| 32 | UVIKO 19 (VACCINE Delivery Support) | 35,985,515.12 | 35,985,515.12 | 100 |
| 33 | Ujenzi wa Madarasa Sekondari (Tozo) | 37,500,000 | 37,500,000 | 100 |
| 34 | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 47 (IMF) | 940,000,000 | 940,000,000 | 100 |
| 35 | Ujenzi wa kituo cha Afya | 250,000,000 | 250,000,000 | 100 |
| 36 | UVIKO 19 (Ufuatiliaji na Tathmini) | 6,514,747 | 6,514,747 | 100 |
| 37 | UVIKO 19 (Vaccine Transfer) | 10,137,391.3 | 10,137,391.3 | 100 |
| 38 | Upimaji wa Ardhi | 1,588,000,000 | 1,588,000,000 | 100 |
| **Jumla wadau wengine wa Maendeleo** | | **7,741,207,010.42** | **4,132,806,167.61** | **53** |
| **Jumla Bajeti ya Halmashauri 2021/2022** | | **40,918,043,040.42** | **22,380,195,433.10** | **55** |

**Tathimini ya mapato ya ndani (Julai – Disemba 2021)**

Halmashauri imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha kunakuwepo na mafanikio ya kutosha katika ukusanyaji wa mapato ya ndani.

**i) Mafanikio katika ukusanyaji wa mapato yametokana na:**

- Kutumia mfumo wa kielektroniki katika kukusanya mapato
- Ugawaji na usambazaji wa hati za madai ya kodi, ada na ushuru mapema.
- Ufuatiliaji wa karibu wa walipa kodi, ada na ushuru unaofanywa na wataalamu wakishirikiana na waheshimiwa madiwani.
- Kutoa elimu ya kodi na matangazo.
- Kutoa motisha kwa walipa kodi wanaolipa kwa wakati bila usumbufu.
- Utozaji kodi kwa kuzingatia muda na sheria.

**ii) Changamoto katika ukusanyaji wa mapato zimetokana na:-**

- Ukosefu wa fedha za fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo yao kunaathiri upimaji viwanja.
- Fedha za Ruzuku kutoka serikali kuu na wafadhili kutolewa kwa kuchelewa/kutototolewa kabisa hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- Ukwepaji wa makusudi wa kulipa kodi, ada na ushuru.
- Walipa kodi kutofahamu sheria ndogo za Halmashauri zinazotawala ukusanyaji mapato.

**iii) Mikakati ya ukusanyaji mapato kwa mwaka 2022/2023**

- Kutafuta fedha kwa ajili ya kulipa fidia za mashamba ili kuweza kupima na kuuza viwanja vingi na kuweza kuongeza mapato yatokanayo na uuzaji viwanja.
- Halmashauri kuendelea kuboresha miundo mbinu wezeshi kama vile ujenzi wa mradi mkakati wa soko la kisasa unaojengwa eneo la kitovu cha Mji na kutafuta eneo la kujenga maegesho ya malori.
- Kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha walipa kodi, ada na ushuru mbalimbali kwa kata zote za Halmashauri ya Mji Kibaha.
- Kuendelea kuboresha takwimu za walipa kodi, ushuru wa huduma, matangazo ya biashara na ushuru wa nyumba za kulala wageni.
- Kuboresha na kuhuisha sheria ndogondogo za ukusanyaji mapato.
- Kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watu wasiotaka kulipa kodi.
- Kufanya ukaguzi wa kodi, ada na ushuru kwa Kata zote mara kwa mara

## 2.2 Mapitio ya Matumizi

### Matumizi Julai – Disemba 2021/2022

Halmashauri ya Mji Kibaha kwa kipindi cha Julai-Disemba 2021 imetumia Jumla ya **Tsh 18,365,770,511.40** sawa na **47.1%** ya Bajeti. Mchanganuo wa Matumizi katika kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2021 umeelezewa katika jedwali Namba 2.2.

Jedwali 2.2: Mapitio ya Makisio ya Mapato na Matumizi Halisi ya Halmashauri kwa Kipindi cha Julai - Disemba, 2021

| No | CHANZO CHA MAPATO | MAKISIO 2020/2021 | MATUMIZI (Julai-Disemba, 2021) | Matumizi Halisi (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya ndani | 4,561,367,650 | 1,921,947,069.47 | 42 |
| | **Jumla Mapato ya Ndani** | **4,561,367,650** | **1,921,947,069.47** | **42** |
| 2 | Ruzuku ya Mishahara | 22,237,022,000 | 12,566,935,240 | 56 |
| 3 | Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida | 1,177,411,380.00 | 767,250,020 | 50 |
| ***Jumla ya Ruzuku ya matumizi Mengineyo (PE&OC)*** | | **23,414,433,380** | **13,334,185,260** | **57** |
| **Ruzuku ya Maendeleo** | | | | |
| 4 | Ujenzi wa soko la kisasa (Mradi Mkakati) | 2,000,000,000 | 489,803,903.92 | 24 |
| 5 | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya | 800,000,000 | 0 | 0 |
| 6 | Ujenzi wa jengo la ofisi ya Halmashauri | 1,000,000,000.00 | 174,732,854 | 17 |
| 7 | Mfuko wa Jimbo | 36,325,000 | 0 | 0 |
| 8 | Ujenzi wa shule ya Sekondari | 1,075,200,000 | 470,000,000 | 44 |
| 9 | Ujenzi wa miundombinu ya elimu Sekondari | 112,500,000 | 112,500,000 | 100 |
| 10 | Uboreshaji wa Elimu (LANES) | 64,510,000 | 0 | 0 |
| 11 | Umaliziaji wa Maboma ya madarasa Elimu Msingi | 112,500,000 | 0 | 0 |
| **Jumla Ruzuku ya Maendeleo** | | **5,201,035,000** | **1,247,036,757.92** | **24** |
| **Wadau wengine wa Maendeleo** | | | | |
| 12 | Michango ya Jamii | 100,000,000 | 52,342,800 | 52 |
| 13 | Mazingira - SWASH | 24,000,000 | 0 | 0 |
| 14 | Ujenzi wa Zahanati | 150,000,000 | 0 | 0 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 15 | Uchaguzi | | | |
| 16 | Ada ya shule Msingi | 135,900,000 | 19,294,865 | 14 |
| 17 | Ada za shule Sekondari | 227,150,000 | 9,196,150.00 | 4 |
| 18 | Elimu-P4R Msingi | 346,581,500 | 0 | 0 |
| 19 | Elimu-P4R Sekondari | 346,581,500 | 0 | 0 |
| 21 | Elimu Bure Msingi | 634,125,620 | 192,268,478.98 | 30 |
| 22 | Elimu Bure Sekondari | 1,447,576,380 | 450,101,125.86 | 31 |
| 23 | TIKA/CHF | 14,000,000 | 2,008,167.17 | 33 |
| 24 | NHIF | 101,909,250 | 41,526,680 | 45 |
| 25 | Kuchangia Papo kwa papo (User Fee) | 142,546,400 | 55.756,792.3 | 43 |
| 26 | Mfuko wa Pamoja Sekta ya Afya | 251,346,000 | 8,881,157 | 20 |
| 27 | Afya-RBF | 329,336,983 | 0 | 0 |
| 28 | Ruzuku ya Afya-THPS | 21,000,000 | 9,530,000 | 45 |
| 29 | Vifaa tiba (MSD) | 283,119,724 | 0 | 0 |
| 30 | TASAF - PSSN | 574,435,000 | 67,500,000 | 12 |
| 31 | UNICEF | 10,000,000 | 0 | 0 |
| 32 | Global Fund | 35,062,000 | 5,390,000 | 15 |
| 33 | NTD | 15,549,000 | 0 | 0 |
| 34 | UVIKO 19 (VACCINE Delivery Support) | 35,985,515.12 | 27,062,000 | 75 |
| 35 | Ujenzi wa madarasa Sekondari (TOZO) | 37,500,000 | 37,500,000 | 100 |
| 36 | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 47 (IMF) | 940,000,000 | 940,000,000 | 100 |
| 37 | Ujenzi wa Zahanati | 250,000,000 | 0 | 0 |
| **Jumla wadau wengine wa Maendeleo** | | **5,912,307,010.42** | **1,862,601,424.01** | **31** |
| **Jumla Bajeti ya Halmashauri 2021/2022** | | **38,952,626,768.12** | **18,365,770,511.40** | **47** |

**2.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Shughuli za Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha Julai –Disemba 2021.**

**2.3.1 IDARA YA UJENZI**

Kazi zilizopangwa kufanyika na zinazoendelea kwa sasa ni:

- Kuendesha mafunzo mbalimbali (Training) pamoja na Ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi (Retooling).

- Ujenzi wa Kituo cha afya Kidimu, Kata ya Pangani. Ujenzi uko katika hatua ya uchimbaji wa msingi.

- Ujenzi wa Kituo cha Afya kongowe. Ujenzi upo katika hatua ya manunuzi, utafutaji wa mafundi wa kujenga na wasambazaji wa vifaa vya ujenzi.

- Ujenzi wa shule ya sekondari Viziwaziwa. Hatua iliyopo ni utambulisho wa ujenzi.

- Ujenzi wa Zahanati ya Sofu. Ujenzi uko katika hatua ya kupaua.

- Ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Sofu. Darasa moja limekamilika, maandalizi ya madarasa mengine yanaendelea.

- Ujenzi wa jengo la Utawala na maabara katika shule ya Sekondari mwambisi. Ujenzi wa msingi umekamilika.

**Majengo**

- Ujenzi wa soko la kisasa eneo la CBD, kazi inaendelea.
- Ujenzi wa Hospital ya wilaya-Lulanzi. Ujenzi upo katika hatua mbalimbali
- Ujenzi wa Kituo cha Afya Kidimu. Ujenzi upo kkatika hatua ya kuchimba msingi
- Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Sofu, darasa 1 limekamilika. Maandalizi ya madarasa mengine yanaendelea.
- Ujenzi wa Zahanati ya Sofu. Ujenzi uko katika hatua ya kupaua.

2.4 **IDARA YA ARDHI NA MALAISILI**

Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni:

- Kuendelea na zoezi la urasimishaji wa makazi holela.

- Uchukuaji wa takwimu za maeneo ya wananchi kwa ajili ya uandaaji wa michoro ya mipangomiji eneo la miradi.

- Kuendelea kutoa elimu ya urasimishaji wa makazi ya wananchi.
- Kuendelea kusimamia na kukagua kazi za urasimishaji wa makazi ya wananchi.
- Kutoa masharti ya uendelezaji wa Ardhi
- Kushughulikia mabadiliko ya matumizi ya ardhi
- Kushughulikia maombi ya vibali vya ujenzi.
- Kuendelea kushirikiana na TRA kutoa elimu ya kodi ya majengo.
- Kufanya marekebisho, kusaini barua za misamaha kabla haijawasilishwa TRA
- Kufanya uthamini kwa madhumuni mbalimbali kama uhamisho wa miliki, fidia, mikopo, kuuza na kununua mali, mirathi, dhamana n.k
- Kuendelea kushughulikia migogoro na malalamko mbalimbali ya ardhi.

### 2.3.1 Maliasili

Kazi zilizofanyika ni:

- Miche ya miti ya aina mbalimbali imeoteshwa na inaendelea kutunzwa katika kitalu cha miche ya miti kwa lengo la kusambazwa katika Taasisi mbalimbali za Serikali, kwa lengo la kuhifadhi mazingira.
- Jumla ya miche ya miti 200 ya kivuli aina ya **"mijohoro na mipera"** ilipandwa katika shule ya Sekondari Picha ya Ndege katika Kata ya Tangini, kwa lengo la kuhifadhi mazingira.

### 2.3.2 Nyuki

**Kazi zilizofanyika ni:**

- Kutembelea na kukagua vikundi vya Nyuki
- Kutoa elimu juu ya namna ya utundikaji bora wa Mizinga
- Kukagua maandiko mbalimbali ya miradi

## 2.5 IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI

Halmashauri Kupitia Idara Ya Mipango, Takwimu Na Ufuatiliaji imeweza kutekeleza shughuli zifuatazo:

- Usimamizi na uratibu wa miradi ya Halmashauri.
- Uandaaji wa Bajeti ya mwaka 2022/2023

- Uandishi wa taarifa mbalimbali zikiwemo taarifa za kila mwezi, taarifa za robo mwaka na taarifa za Utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi
- Ukaguzi wa miradi ya Maendeleo
- Kuhudhuria vikao mbalimbali vya kisheria
- Uandishi wa Miradi ya Maendeleo

## 2.6 IDARA YA ELIMU SEKONDARI

Idara ya Elimu Sekondari katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2021 imetekeleza shughuli zifuatazo:

### 2.3.2 Idara ya Elimu Sekondari

Kazi zilizofanyika katika idara ya Elimu sekondari ni pamoja na;

- Maafisa wa idara ya Elimu Sekondari walitembelea shule za sekondari Mwanalugali, Bundikani, Visiga, Mbwawa Miswe, Mwambisi Forest, Pangani, Miembesaba, Nyumbu, Tumbi, Kibaha, Kidimu, Simbani, Kibaha Girls, Zogowale, Msangani Government na Picha ya Ndege kufuatilia maendeleo ya taaluma na kusimamia walimu na kuhakikisha wanamaliza mihtasariyao kwa wakati.
- Kuandaa na kushiriki kikao cha wadau wa Elimu 15/09/2021. Idara ya elimu sekondari na Msingi lilishirikiana katika kufanya maandalizi ya kikao cha wadau wa Elimu
- Kuandaa semina ya walimu wa sayansi wa masomo ya FIZIKIA,KEMIA, BIOLOJIA NA KILIMO.Tarehe 22/09/2021
- Kushiriki katika maandalizi na usambazaji wa Mtihani wa kumaliza Elimu ya msingi 2021
- Kukusanya taarifa za LAAC kutoka mashuleni na kuiunganisha.
- Kupokea, kuandaa na kutuma taarifa mbalimbali nje na ndani ya Halmashauri.
- Kuendelea kupokea uhamisho na kuhamisha wanafunzi kutoka na kwenda shule zingine kwenye mfumo wa prems.
- Kupokea mchanganuo wa fedha za elimu bila malipo na ufuatiliaji matumizi yake kwa kuhakikisha shule sekondari za serikali zinazingatia mwongozo wa matumizi kwa kufuata asilimia zilizopangwa na ofisi ya Rais TAMISEMI.
- Kuratibu na kusimamia mtihani wa pre-National kidato cha nne 2021.

- Kuwapeleka wakazi katika ziara ya ukaguzi wa miradi mbalimbali iliyotekelezwa na idara ya Elimu

## 2.7 IDARA YA ELIMU MSINGI

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba, 2021 Idara ya Elimu Msingi iliendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

- Uhamisho wa wanafunzi katika mfumo wa PREM ambapo wastani wa wanafunzi 45-55 kwa siku huhamishwa na kupokelewa.
- Kikao cha Maafisa Elimu wa Idara, walimu wakuu na wamiliki wa Shule Binafsi kilifanyika tarehe 8.12.2021 kwa lengo la Kutathimini Matokeo ya Mtihani wa Taifa wa darasa la Saba 2021. Jumla ya wanafunzi 4747 walisajiliwa kufanya Mtihani ambapo walikuwa wav.2375 na was 2372. Wanafunzi waliofanya Mtihani walikuwa 4739 wav 2371 na was 2368. Waliofaulu ni 4514 wav ni 2265 na was 2249 sawa na Asilimia 95.25. Aidha mkakati wa uboreshaji wa Taaluma 2022 ulijadiliwa na kupangwa.
- Kufanyika kwa kikao kazi kilichowahusisha Wamiliki wote wa Shule binafsi zikiwemo taasisi za Dini siku ya tarehe 13/12/2021 lengo likiwa ni kuelekeza utekelezaji wa Miongozo inayotolewa na serikali juu ya uendeshaji na usimamizi bora wa shule.
- Uchambuzi wa wanafunzi kuingia kidato cha kwanza 2022 ambapo jumla ya wanafunzi 4514 sawa na Asilimia 95.25 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 2022 katika Shule za serikari wakiwemo wav 2265 na was 2249. Miongoni mwao wapo wanafunzi 6 wenye mahitaji maalum, wakiwemo wavulana 04 na wasichana 02 nao wamechaguliwa katka shule Maalum.
- Maafisa Elimu kutembelea Shule na Kuandaa taarifa ya ufuatiliaji wa ufundishaji na ujifunzaji. Shule hizo zilizotembelewa zilikuwa ni Fabcast, Al-fulqaan, Bungo, kidimu na Vikawe.
- Kuandaa na kusimamia Mtihani wa Muhula wa II kwa masomo na madarasa yote ambapo mitihani hiyo ilianza tarehe 23/11/2021 hadi 26/11/2021. Aidha shughuli ya kupokea na kuunganisha matokeo ya mtihani huo kwa Shule zetu zote imekamilika tayari.
- Maafisa Elimu Taaluma kuhudhuria mafunzo ya Uthibiti Ubora wa Shule wa ndani tarehe 3 Desemba 2021. Mafunzo yalifanyika Morogoro.

- Kutoa mafunzo ya siku tatu 3 kwa Maafisa Elimu Kata, wakuu wa shule na walimu wa Takwimu. Tarehe 6/12/2021 hadi 8/12/2021 Maafisa Elimu kata 14 na Walimu wakuu 73 walihudhuria mafunzo ya Uthibiti Ubora wa ndani wa Shule katika ukumbi wa kibaha sekondari kwa lengo la kujengewa uwezo. Aidha tarehe 16 hadi 17/12 mafunzo ya Mfumo wa PREM na SIS yalitolewa kwa Maafisa Elimu kata 14, Walimu wakuu 73 na walimu wa takwimu 73 na walimu wa madarasa lengo ikiwa ni kuimarisha usimamizi wa ufundishaji, taarifa na takwimu.
- Kufanyika kwa Mtihani wa Upimaji wa kitaifa darasa la IV SFNA 2021 ambapo kwa ratiba ya mtihani huo wa Upimaji ulifanyika kuanzia tarehe 28/10/2021 hadi tarehe 29/10/2021 kama ilivyokuwa imepangwa na kutekelezwa katika ratiba iliyotolewa na baraza la mitihani Taifa.
- Kuingiza data katika Mfumo wa SIS ambapo jumla ya vyandarua 12,074 vilizosambazwa na taarifa ziliingizwa katika Mfumo.
- Kuandaa Tange ya Walimu, ambapo jumla ya walimu 891 waliingizwa kwenye Tange ya Idara ya Elimu Msingi.
- Kuandaa Takwimu ya walimu na kuhakiki mishahara yao kila ifikapo kati ya tarehe 16 hadi 20 ya mwezi ambapo zoezi zima kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba limekuwa likikamilika vema na kuwasilishwa utumishi.
- Kufanya Maandalizi ya Bajeti ya Idara ya Elimu Msingi ya Mwaka 2021/2022. Bajeti ya mishahara ya Watumishi walimu imekamilika, aidha Maandalizi ya bajeti ya Ruzuku inaendelea.
- Mapokezi na usambazaji wa vitabu vya Elimu ya Awali na Elimu msingi kutoka katika serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya shule zake za serikali ambapo mapokezi na ugawaji ulifanyika tarehe 19/12/2021 hadi 28/12/2021.
- Kuratibu na kushiriki maandalizi ya michezo ya 14 ya Taifa kwa watu wenye ulemavu wa Akili (Special Olympics) ambayo ilifanika jijini M wanza tarehe 13-17/12/2021. Maandalizi na ufanyikaji wa Michezo hiyo Kimkoa ilifanyika tarehe 6/12/2021 hadi 12/12/2021 katika viwanja vya Kibaha sekondari ambapo wanafunzi 6 wenye ulemavu wa Akili kutoka vitengo vya Akili vya shule ya msingi mkoani, kongowe na Mailimoja walishiriki masindano.

- Kufanyika kwa Maadhimisho ya siku ya "Fimbo Nyeupe" kitaifa kwa watu wasioona katika viwanja vya stendi ya zamani ya Mailimoja kuanzia tarehe 04.11.2021 hadi 05.11.2021 ambapo mgeni rasmi katika siku ya Kilele cha Maadhimisho alikuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu-Watu wenye Ulemavu Mh. Ummy Ndelinanga
- Kuandaa ikama ya walimu wataalam wa Elimu maalumu Msingi kwa fani(Specializations) walizosomea. Hali ya ikama Elimu Maalum Msingi ni Mahitaji 42-45 waliopo 21 upungufu 32-35. Hata hivyo wataalamu 4 wamepewa majukumu ya kiutawala na hivyo upungufu Halisi ni 36-39.
- Maandalizi ya taarifa ya idadi ya shule zote za serikali zinazotoa huduma ya Elimu Maalum katika Mfumo wa vitengo, Maalumu na Jumuishi na kuiwasilisha kwa katibu tawala Mkoa tarehe 27/11/2021 hadi 28/11/2021. Hadi sasa zipo shule 40 za Msingi za Elimu maalum ambapo 3 hutoa huduma kwa Vitengo na 37 hutoa Elimu kwa mfumo Jumuishi. Aidha shule 8 kati ya 16 za Sekondari za serikali zimepokea Wanafunzi wenye mahitaji Maalum na kuwahudumia katika Mfumo Jumuishi. Changamoto ni upungufu mkubwa wa walimu wataalamu.
- Kukusanya Maoteo ya uandikishaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji Maalum wa Elimu ya Awali na Drasa la Kwanza 2022. Katika takwimu hizo Elimu ya Awali ni wanafunzi 215 wakiwemo wavulana 112 na wasichana 103 Darasa la Kwanza ni 208 wakiwemo wavulana 105 na wasichana 103.
- Kukusanya, kupitia na kuchambua taarifa na Takwimu za Awali za wanafunzi wenye Mahitaji Maalum na walimu wataalam wa Elimu Maalum kwa lengo la kuhuwisha na kuimarisha mfumo wa Takwimu za Elimu Maalumu kama zilivyohitajika na OR-TAMISEMI mnamo mwezi Novemba na Desemba 2021.
- Kufanyika kwa Tamasha la uhamasishaji wa upatikanaji wa chakula Shuleni tarehe 15/11/2021 katika Shule ya Msingi Kongowe ambapo mgeni Rasmi alikuwa Mh. Mkuu wa Wilaya ya Kibaha Mh Sara Msafiri
- Afisa Elimu Sayansikimu Kuandaaa makisio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 ya utekelezaji washuguli za huduma ya Afya, Maji, Usafi wa Mazingira na Usafi binafsi shuleni.

- Kutembelea Wanafunzi wa MUKEJA 120 Me 3 Ke 117 Mwendapole. Wanakisomo walifanyiwa tathmini ya maendeleo yao kupitia Mtihani. Hata hivyo changamoto ni ukosefu wa vifaa vya kufundishia katika kituo hicho.
- Kutembelea Vituo 12 vyenye wanafunzi wa MEMKWA lengo ni kupata idadi ya waliokuwepo na kuwasajili wanaostahili kufanya mtihani wa kitaifa darasa la nne 2021.
- Kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na Matundu ya vyoo.Ufuatiliaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Tumbi, maendeleo, Saeni(mpya), Mkombozi(Mpya), Nkwabi(Mpya), Karabaka(Mpya) na Mkoani. Aidha ufuatiliaji wa ujenzi wa Matundu ya Vyoo ulifanyika katika shule ya Msingi Jitihada, Bungo, Mailimoja, Maendeleo, na Lumumba.
- Kufuatilia na kusambaza Madawati 916 kwa Shule ya sekondari Visiga, Mwambisi, Simbani, Miembesaba, Nyumbu, Bundikani na Kidimu.
- Kufanyika kwa Ziara ya michezo ya kirafiki baina ya Halmashauri ya Mji Kibaha na Halmashauri ya wilaya ya Bagamoyo iliyofanyika tarehe 8/12/2021. Michezo ya mpira wa wavu, soka na Netiboli ilifanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.
- Mashindano ya Special Olympics. Michezo ya Watu wenye ulemavu imefanyika kimkoa kuanzia tarehe 9-12/12/2021 katika viwanya vya Shirika la Elimu kibaha. Mashindano hayo kitaifa yalifanyika Jijini Mwanza tumeshiriki mashindano hayo kuanzia tarehe 13-17/12/2021. Timu ya mkoa wa Pwani iliibuka na Medali 12(Dhahabu 7, Shaba 1, na Fedha 4) na Liboni 15.

- Vibali mbalimbali 206 vyenye thamani ya Tsh. 4,050,000.00 vilitolewa kwa wateja.
- Kusajili Filamu moja ya kikundi cha Mkombozi, pia kusajili kikundi kimoja cha Mkulima.
- Kuratibu Mashindano ya Insha ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara kwa wanafunzi wa Shule za Msingi.
- Kuratibu mazoezi ya viungo pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya tarehe 13/11/2021.
- Mazoezi ya viungo na wanafunzi wa shule ya sekondari west Gate tarehe 12/11/2021

- Ufuatiliaji wa uimbaji wa nyimbo za Uzalendo kama zinafundishwa Shuleni ipasavyo, pamoja na kuhakikisha kuwa Bendera na picha ya Rais zipo shuleni.

### 2.3.3 Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika

Kazi zilizofanyika idara ya Kilimo, umwagiliaji na ushirika ni pamoja na;

- Kusimamia uokotaji, ukaushaji na kushauri uuzaji wa korosho katika mfumo wa stakabadhi ghalani.
- Kutoa ushauri wa kilimo bora cha mazao ya chakula, bustani na biashara ambapo jumla ya wakulima 2,336 wamepata ushauri
- Kuhamasisha vijana kushiriki ujenzi wa kitalu nyumba ambapo jumla ya vijana 20 wameshiki katika ujezi wa kitalunyumba katika eneo la Zegereni.
- Kukusanya takwimu za mwenendo wa upatikanaji wa chakula.
- Kutoa elimu ya kilimo cha mchicha na ugawaji wa mbegu bora za mchicha ambapo jumla ya wakulima 160 wamegawiwa mbegu bora za Mchicha kupitia watafiti wa ARI Mikocheni.
- Kuwashauri wakulima namna bora ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi kutokana na taarifa za hali ya hewa za kuchelewa kwa mvua za vuli.

### 2.3.4 Idara ya Mifugo na Uvuvi

Kazi zilizofanyika idara ya Mifugo na uvuvi ni pamoja na;

- Kutoa ushauri, elimu na kuwahamasisha wafugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, mbwa na samaki kuhusu ufugaji bora na wenye tija
- Kufanya huduma mbalimbali, kinga na tiba kwa mifugo dhidi ya magonjwa mbalimbali
- Kufanya ukaguzi wa nyama katika machinjio ya Mtakuja-Pangani na katika masoko ya nyama choma kata ya Tangini na Sofu
- Kukusanya takwimu mbalimbali zinazohusu idara ya mifugo na uvuvi na kuandaa taarifa husika
- Kuendeleza shughuli za kitengo cha uvuvi

### 2.3.5 Idara ya Afya

Kazi zilizofanyika idara ya Afya ni pamoja na;

- Kuratibu shughuli za VVU/UKIMWI

- Kuratibu shughuli za Uzazi na Mtoto
- Kuratibu shughuli za Malipo kwa Ufanisi (RBF)
- Kuratibu shughuli za Maabara
- Kuratibu shughuli za utoaji wa dawa
- Kuratibu shughuli za Chanjo
- Huduma nyingine

Aidha Idara ya Afya imetekeleza huduma nyingine kama ifuatavyo:

- Huduma ya Uuguzi
- Huduma ya magonjwa yasiyoambukiza
- Huduma za macho
- Huduma za kifua kikuu, UKIMWI na Ukoma
- Huduma za Kinga na Afya Mazingira
- Huduma za Lishe
- Huduma za Ustawi wa Jamii

### 2.3.7 Idara ya Maendeleo ya Jamii

Kazi zilizofanyika idara ya Maendeleo ya jamii ni pamoja na;

- Kufuatilia marejesho kwenye vikundi vya Vijana na wanawake wajasiriamali.
- Kuhamasisha wananchi kujikinga na kuchukua tahadhari juu ya maambukizi ya COVID 19
- Uratibu wa shughuli za Malalamiko
- Uratibu na Usajili wa AZAKI ( Asasi za Kijamii ) na AZISE (Asasi zisizo za Kiserikali).
- Kuratibu dawati la Uwezeshaji Wananchi kiuchumi
- Uratibu wa shughuli za Vijana
- Usajili wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za kifedha (CMGs)

Kazi zilizotekelezwa nje ya mpango kazi ni kama ifuatavyo:

- Kufanya kikao na kutoa elimu kwa Wajasiriamali wote waliopata mkopo kupitia mfuko wa WDF, YDF na walemavu juu ya umuhimu wa kuwa na vitambulisho vya ujasiriamali katika kutekeleza shughuli zao za ujasiriamali.

- Kuhamasisha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kusajili vikundi vya Ujasiriamali, kufungua akaunti benki, kuandika michanganuo na kuomba mkopo wa YDF, WDF na watu wenye ulemavu.

### 2.3.8 Kitengo cha Usafi na Mazingira

Kazi zilizofanyika kitengo cha usafi na mazingira ni pamoja na;

- Kusimamia agizo la Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kufanya usafi kila ifikapo Jumamosi ya mwisho ya kila Mwezi.
- Kusimamia hifadhi na utunzaji wa mazingira katika uchimbaji wa madini ujenzi (mchanga).
- Kusimamia usafi wa mazingira ikiwemo ukusanyaji, uzoaji na usafirishaji wa taka ngumu kwenda dampo.
- Kusimamia uzikaji wa miili ya marehemu wasiojulikana.
- Ukaguzi wa viwanda

## 2.12 Changamoto na Mikakati katika utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022

### 2.12.1 Changamoto

Pamoja na Halmashauri ya Mji kupata mafanikio makubwa katika utoaji wa huduma kwa wananchi bado kumekuwepo na changamoto mbalimbali zilizojitokeza na hivyo kuathiri utendaji wa baadhi ya majukumu yake. Baadhi ya changamoto hizo ni:

i. Ucheleweshwaji wa fedha toka serikali kuu.
ii. Uchangiaji hafifu wa jamii katika miradi.
iii. Upungufu wa watumishi hasa katika Idara ya Ujenzi.
iv. Kupasuka kwa majengo kutokana na hali halisi ya ardhi ya Mji wa Kibaha, Sehemu kubwa ni udongo wa mfinyanzi ambao huhitaji aina ya msingi wa kumwaga jamvi sehemu yote ya jengo. Ujenzi huu ni gharama kubwa sana nao si rahisi kukubalika kwa wananchi wengi na hata Taasisi za Umma kutokana na fedha kidogo zinazotolewa.
v. Tatizo la viwanja kutoendelezwa kwa wakati ambapo inaikosesha Halmashauri mapato.
vi. Kutokuwa na ardhi huru ya kupima viwanja kutokana na uhaba wa fedha za kulipa fidia

vii. Upungufu wa vitendea kazi kama vile vifaa vya upimaji na samani za ofisi za kuchorea.

viii. Kukauka kwa baadhi ya vyanzo vya maji kutokana na uharibifu wa mazingira unaofanyika katika jamii.

ix. Baadhi ya changamoto zinazoikabili Sekta ya Ujenzi katika Halmashauri ya Mji Kibaha ni kama hizi zifuatazo: -

Wananchi kuendelea na ujenzi bila ya kuwa na vibali vya ujenzi licha ya elimu kutolewa na operation za mara kwa mara za ukaguzi.

x. Baadhi ya wananchi kukwepa kulipa kodi kupelekea Halmashauri kukosa mapato

### 2.12.2 Mikakati

i. Kuendelea kuhamasisha jamii juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kupanda miti

ii. Kuendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili kutuma fedha kwa wakati

iii. Kuendelea kuhamasisha wananchi kuchangia miradi ya maendeleo inayojengwa katika maeneo yao ili kujenga umiliki wa miradi hiyo na kuitunza.

iv. Kuhamasisha matumizi endelevu ya maliasili ikijumuisha matumizi endelevu ya ardhi hasa uratibu wa maendeleo ya makazi yaliyopimwa.

v. Halmashauri inapanga kusimamia kwa karibu kazi zote za ujenzi wa Majengo kwa kutumia vifaa vilivyopo ili kuhakikisha Majengo yanajengwa (kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu) kwa ubora unaotakiwa ili wananchi wa Mji wa Kibaha waweze kujiletea maendeleo yao haraka.

vi. Kuendelea kushirikiana na Waheshimiwa madiwani, viongozi wa Kata, Mitaa, ambako miradi ya ujenzi inafanyika ili kuongeza nguvu katika kusimamia maendeleo ya miradi hiyo.

vii. Kuendelea kushirikiana na uongozi wa Wilaya na Mkoa katika kusisitiza wamiliki kuendeleza viwanja vyao.

viii. Halmashauri inaendelea kutenga fedha za ulipaji fidia pamoja na ununuzi wa vitendea kazi. ili kutekeleza majukumu yake na kupambana na changamoto zilizoorodheshwa hapo juu,

ix. Kuendelea kushirikiana na kamati za shule, Viongozi wa Mitaa, ambako miradi ya majengo inatekelezwa ili kuongeza nguvu katika kusimamia maendeleo ya miundombinu hiyo.

x. Kuendelea na uhamasishaji kwa viongozi ili waweze kushawishi wananchi wachangie miradi iliyo katika maeneo yao.
xi. Kuendelea kuomba vitendea kazi na watumishi ili kazi zisikwame Kuendelea kushirikiana na kamati za shule, Viongozi wa Mitaa, ambako miradi ya majengo inatekelezwa ili kuongeza nguvu katika kusimamia maendeleo ya miundombinu hiyo.
xii. Kuendelea na uhamasishaji kwa viongozi ili waweze kushawishi wananchi wachangie miradi iliyo katika maeneo yao.
xiii. Kuendelea kuomba vitendea kazi na watumishi ili kazi zisikwame.
xiv. Halmashauri inaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili waweza kulipa kodi kwa hiari.

SURA YA TATU

## 3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA PAMOJA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023

### 3.1 Makisio ya Mapato kwa Mwaka 2022/2023

Halmashauri ya Mji kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imekadiria kukusanya na kupokea jumla ya **Shilingi 45,832,490,885.50** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikali Kuu na mapato ndani. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,321,184,910.99** ni kutoka vyanzo vya ndani ambapo shilingi shilingi , shilingi **41,511,305,974.51** ni ruzuku kutoka serikali kuu kati ya fedha hizo mishahara Tshs **31,975,459,680.00** matumizi ya kawaida Tshs **1,065,750,098.83**, fedha za Miradi ya Maendeleo Tshs **8,470,096,195.68**. Aidha, Tshs **425,624,988** ni mapato ya vyanzo fungwa na mchango wa jamii kama ifuatavyo: **Tshs 120,000,000** ni mchango wa jamii katika shughuli za maendeleo**, Tshs 18,649,257.56** kutoka iCHF, **Tshs 110,399,330** kutoka NHIF na Tshs **176,576,400.12** malipo ya papo kwa papo (User Fee), (Tazama jedwali hapo chini 3a & b)

**Jedwali 3a: Muhtasari wa Makisio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka 2022/2023**

| **Kasma** | | **Chanzo Cha Mapato** | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| | | **Mapato ya Ndani** | **Ruzuku Toka Serikali Kuu** | |
| 1. Mishahara | | **0** | **31,975,459,680.00** | **31,975,459,680.00** |
| 2. Matumizi ya Kawaida (OC) | | | | |
| 500 A | Utawala | 689,898,000.00 | 166,657,000.00 | 856,555,000.00 |
| 501A | Usafi wa mazingira | 125,000,000.00 | 0 | 125,000,000.00 |
| 502A | Fedha | 390,000,000.00 | 0 | 390,000,000.00 |
| | Biashara | 45,000,000.00 | 0 | 45,000,000.00 |
| 503A | Mipango na | 271,039,199.40 | 0 | 271,039,199.40 |

| Kasma | | Chanzo Cha Mapato | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Mapato ya Ndani | Ruzuku Toka Serikali Kuu | |
| | Uchumi | | | |
| 505B | Mifugo | 90,000,000.00 | 12,082,000.00 | 102,082,000.00 |
| 506B | Kilimo | 55,000,000.00 | 12,124,000.00 | 67,124,000.00 |
| 506D | Ushirika | 10,000,000.00 | 0 | 10,000,000.00 |
| 507A | Elimu msingi-Utawala | 18,560,000.00 | 429,758,000.00 | 448,318,000.00 |
| 507E | Utamaduni na Michezo | 26,000,000.00 | 0 | 26,000,000.00 |
| 507F | Elimu-Usafi wa Mazingira | 41,328,000.00 | 0 | 41,328,000.00 |
| 507G | Elimu-TSD | | 0 | 0.00 |
| 509B | Elimu Sekondari (OC) | 25,000,000.00 | 329,639,098.83 | 354,639,098.83 |
| 511A | Ujenzi | 40,000,000.00 | 18,034,000.00 | 58,034,000.00 |
| 512B | Mipango Miji (Ardhi) | 80,000,000.00 | 0 | 80,000,000.00 |
| 512F | Maliasili | 15,000,000.00 | 0 | 15,000,000.00 |
| 514A | Sheria | 50,000,000.00 | 0 | 50,000,000.00 |
| 515A | Ukaguzi wa ndani | 60,000,000.00 | 0 | 60,000,000.00 |
| 516A | Ugavi | 45,000,000.00 | 0 | 45,000,000.00 |
| 518A | Teknologia ya Habari na Mawasiliano | 65,000,000.00 | 0 | 65,000,000.00 |
| 519A | Nyuki | 10,000,000.00 | 0 | 10,000,000.00 |
| 527A | Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto | 135,000,000.00 | 0 | 135,000,000.00 |

| Kasma | | Chanzo Cha Mapato | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Mapato ya Ndani | Ruzuku Toka Serikali Kuu | |
| | UKIMWI | 40,000,000.00 | 0 | 40,000,000.00 |
| 508D | Afya-CHMT | 65,000,000.00 | 78,896,000.00 | 143,896,000.00 |
| | Kituo cha Afya | 0 | 0 | 0.00 |
| 508E | Afya-Zahanati | 30,000,000.00 | 0 | 30,000,000.00 |
| | Afya-Ustawi wa Jamii | 70,000,000.00 | 0 | 70,000,000.00 |
| | Afya-Lishe | 30,000,000.00 | 0 | 30,000,000.00 |
| | Afya-Hospitali ya Wilaya | 20,000,000.00 | 0 | 20,000,000.00 |
| 510A | Maji | 0 | 0 | 0.00 |
| 517A | Uchaguzi | 40,000,000.00 | 0 | 40,000,000.00 |
| **Jumla ndogo matumizi ya Kawaida (OC)** | | **2,581,826,399.40** | **1,065,750,098.83** | **3,647,576,498.23** |
| **JUMLA MISHAHARA NA MATUMIZI YA KAWAIDA** | | **2,581,826,399.40** | **32,337,999,680.00** | **35,623,036,178.23** |

**Jedwali 3b. Mapato ya Fedha za Miradi ya Maendeleo 2022/2023**

| *Na* | Chanzo cha Mapato | Mapato 2022/2023 |
|---|---|---|
| 1. | Mapato ya Ndani | 1,739,359,711.59 |
| | **Jumla ndogo Mapato ya Ndani** | **1,739,359,711.59** |
| 2. | Mchango wa Jamii | 120,000,000.00 |
| 3. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya | 800,000,000 |
| 4. | Ujenzi wa Zahanati | 150,000,000 |
| 5. | Tanzania Health Promotion Support-THPS | 21,000,000.00 |
| 6. | Fedha za Ruzuku (CAPITATION) Elimu Msingi | 217,884,000.00 |

| *Na* | Chanzo cha Mapato | Mapato 2022/2023 |
|---|---|---|
| 7. | Fedha za Ruzuku (CAPITATION) Elimu Sekondari | 137,000,000.00 |
| 8. | Ruzuku ya Madaraka Elimu Msingi | 147,600,000.00 |
| 9. | Ruzuku ya Madaraka Elimu Sekondari | 48,000,000.00 |
| 10. | Fedha za Mitihani Elimu Msingi | 202,112,620.00 |
| 11. | Fedha za Mitinahi Elimu Sekondari | 420,367,380.00 |
| 12. | Fedha ya chakula Elimu Msingi | 66,528,000.00 |
| 13. | Fedha ya chakula Elimu Sekondari | 615,060,000.00 |
| 14. | Fedha za uboreshaji Elimu Msingi (LANES) | 32,255,000.00 |
| 15. | Fedha za uboreshaji Elimu Sekondari (LANES) | 32,255,000.00 |
| 16. | Kampeni ya Taifa ya Usafi | 24,000,000.00 |
| 17. | Fedha za umaliziaji wa Maboma ya Madarasa | 112,500,000.00 |
| 18. | Fedha za uboresheaji wa Miundombinu ya Elimu Sekondari | 237,500,000.00 |
| 19. | Fidia ya Ada Elimu Sekondari | 227,150,000.00 |
| 20. | P4R | 693,163,000.00 |
| 21. | TASAF | 574,435,000.00 |
| 22. | Mfuko wa Pamoja (HSBF) | 251,346,000.00 |
| 23. | Child Survival Development program UNICEF Grant | 10,000,000.00 |
| 24. | Ujenzi wa Jengo la Halmashauri | 1,000,000,000 |
| 25. | Mfuko wa Jimbo | 36,325,000.00 |
| 26. | Vyanzo Vingine (User Fee, iCHF na NHIF) | 305,624,987.68 |
| 27. | Global Fund | 86,826,000.00 |
| 28. | NTD | 21,164,208.00 |
| 29. | Mradi Mkakati wa Kuongeza Mapato, Soko la Kisasa (CBD). | 2,000,000,000 |
| **Jumla Ruzuku ya Maendeleo** | | **8,470,096,195.68** |
| **Jumla Miradi ya Maendeleo Ruzuku na Michango ya Jamii** | | **8,590,096,195.68** |
| **JUMLA KUU MIRADI YA MAENDELEO** | | **10,329,455,907.27** |

## 4.0 MATUMIZI

Halmashauri ya Mji Kibaha kwa Mwaka 2022/2023 inakadiria kutumia Jumla ya **Tsh 45,832,490,885.50** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato.

**Mapato ya ndani**

Mapato ya ndani **Tsh 4,321,184,910.99** kati ya fedha hizo **Tsh 2,581,826,399.40** sawa na **59.7%** zitatumika kugharamia uendeshaji wa shughuli za Ofisi na utoaji wa huduma, **Tsh 1,739,359,711.59** sawa na **40.3%** zitatumika kutekeleza miradi ya maendeleo. Ziada 1,200

**Ruzuku kutoka Serikali kuu.**

Halmashauri inategemea kutumia **Tsh 41,511,305,974.51,** kati ya fedha hizo Mishahara ni **Tsh 31,975,459,680** sawa n**a 77%,** Matumizi mengineyo **Tsh 1,065,750,098.83** sawa n**a 2.6%,** Miradi ya maendeleo toka kwa wafadhili wengine **Tsh 8,470,096,195.68,** sawa na **20.4%**.

**Matumizi kutoka kwa wadau wengine wa maendeleo.**

Halmashauri inategemea kutumia Shilingi **425,624,988** kutoka kwa wadau wengine wa maendeleo kwa mchanganuo ufuatao, Malipo ya papo kwa papo (User Fee) shilingi **176,576,400.12**, NHIF shilingi **110,399,330.00** na Mchango wa Jamii katika miradi ya maendeleo shilingi **120,000,000**.

**Jedwali 4 a): Matumizi ya Kawaida (OC) na Mishahara kwa Mwaka 2022/2023**

| Kasma | | Chanzo Cha Mapato | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | **Makisio ya Matumizi ya Mapato ya Ndani** | **Makisio ya Matumizi ya Ruzuku Toka Serikali Kuu** | |
| 1. Mishahara | | **0** | **31,975,459,680.00** | **31,975,459,680.00** |
| 2. Matumizi ya Kawaida (OC) | | | | |
| 500 A | Utawala | 689,898,000.00 | 166,657,000.00 | 856,555,000.00 |
| 501A | Usafi wa mazingira | 125,000,000.00 | 0 | 125,000,000.00 |
| 502A | Fedha | 390,000,000.00 | 0 | 390,000,000.00 |

| Kasma | | Chanzo Cha Mapato | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Makisio ya Matumizi ya Mapato ya Ndani | Makisio ya Matumizi ya Ruzuku Toka Serikali Kuu | |
| | Biashara | 45,000,000.00 | 0 | 45,000,000.00 |
| 503A | Mipango na Uchumi | 271,039,199.40 | 0 | 271,039,199.40 |
| 505B | Mifugo | 90,000,000.00 | 12,082,000.00 | 102,082,000.00 |
| 506B | Kilimo | 55,000,000.00 | 12,124,000.00 | 67,124,000.00 |
| 506D | Ushirika | 10,000,000.00 | 0 | 10,000,000.00 |
| 507A | Elimu msingi-Utawala | 18,560,000.00 | 429,758,000.00 | 448,318,000.00 |
| 507E | Utamaduni na Michezo | 26,000,000.00 | 0 | 26,000,000.00 |
| 507F | Elimu-Usafi wa Mazingira | 41,328,000.00 | 0 | 41,328,000.00 |
| 507G | Elimu-TSD | | 0 | 0.00 |
| 509B | Elimu Sekondari (OC) | 25,000,000.00 | 329,639,098.83 | 354,639,098.83 |
| 511A | Ujenzi | 40,000,000.00 | 18,034,000.00 | 58,034,000.00 |
| 512B | Mipango Miji (Ardhi) | 80,000,000.00 | 0 | 80,000,000.00 |
| 512F | Maliasili | 15,000,000.00 | 0 | 15,000,000.00 |
| 514A | Sheria | 50,000,000.00 | 0 | 50,000,000.00 |
| 515A | Ukaguzi wa ndani | 60,000,000.00 | 0 | 60,000,000.00 |
| 516A | Ugavi | 45,000,000.00 | 0 | 45,000,000.00 |
| 518A | Teknologia ya Habari na Mawasiliano | 65,000,000.00 | 0 | 65,000,000.00 |

| Kasma | | Chanzo Cha Mapato | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Makisio ya Matumizi ya Mapato ya Ndani | Makisio ya Matumizi ya Ruzuku Toka Serikali Kuu | |
| 519A | Nyuki | 10,000,000.00 | 0 | 10,000,000.00 |
| 527A | Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto | 135,000,000.00 | 0 | 135,000,000.00 |
| | UKIMWI | 40,000,000.00 | 0 | 40,000,000.00 |
| 508D | Afya-CHMT | 65,000,000.00 | 78,896,000.00 | 143,896,000.00 |
| | Kituo cha Afya | 0 | 0 | 0.00 |
| 508E | Afya-Zahanati | 30,000,000.00 | 0 | 30,000,000.00 |
| | Afya-Ustawi wa Jamii | 70,000,000.00 | 0 | 70,000,000.00 |
| | Afya-Lishe | 30,000,000.00 | 0 | 30,000,000.00 |
| | Afya-Hospitali ya Wilaya | 20,000,000.00 | 0 | 20,000,000.00 |
| 510A | Maji | 0 | 0 | 0.00 |
| 517A | Uchaguzi | 40,000,000.00 | 0 | 40,000,000.00 |
| **Jumla ndogo matumizi ya Kawaida (OC)** | | **2,581,826,399.40** | **1,065,750,098.83** | **3,647,576,498.23** |
| **JUMLA MISHAHARA NA MATUMIZI YA KAWAIDA** | | **2,581,826,399.40** | **32,337,999,680.00** | **35,623,036,178.23** |

Jedwali 4b Matumizi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo 2022/2023

| *Na* | Chanzo cha Mapato | Mapato 2022/2023 |
|---|---|---|
| 1. | Mapato ya Ndani | 1,739,359,711.59 |
| | **Jumla ndogo Mapato ya Ndani** | **1,739,359,711.59** |
| 2. | Mchango wa Jamii | 120,000,000.00 |
| 3. | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya | 800,000,000 |
| 4. | Ujenzi wa Zahanati | 150,000,000 |
| 5. | Tanzania Health Promotion Support-THPS | 21,000,000.00 |
| 6. | Fedha za Ruzuku (CAPITATION) Elimu Msingi | 217,884,000.00 |
| 7. | Fedha za Ruzuku (CAPITATION) Elimu Sekondari | 137,000,000.00 |
| 8. | Ruzuku ya Madaraka Elimu Msingi | 147,600,000.00 |
| 9. | Ruzuku ya Madaraka Elimu Sekondari | 48,000,000.00 |
| 10. | Fedha za Mitihani Elimu Msingi | 202,112,620.00 |
| 11. | Fedha za Mitinahi Elimu Sekondari | 420,367,380.00 |
| 12. | Fedha ya chakula Elimu Msingi | 66,528,000.00 |
| 13. | Fedha ya chakula Elimu Sekondari | 615,060,000.00 |
| 14. | Fedha za uboreshaji Elimu Msingi (LANES) | 32,255,000.00 |
| 15. | Fedha za uboreshaji Elimu Sekondari (LANES) | 32,255,000.00 |
| 16. | Kampeni ya Taifa ya Usafi | 24,000,000.00 |
| 17. | Fedha za umaliziaji wa Maboma ya Madarasa | 112,500,000.00 |
| 18. | Fedha za uboresheaji wa Miundombinu ya Elimu Sekondari | 237,500,000.00 |
| 19. | Fidia ya Ada Elimu Sekondari | 227,150,000.00 |
| 20. | P4R | 693,163,000.00 |
| 21. | TASAF | 574,435,000.00 |
| 22. | Mfuko wa Pamoja (HSBF) | 251,346,000.00 |
| 23. | Child Survival Development program UNICEF Grant | 10,000,000.00 |
| 24. | Ujenzi wa Jengo la Halmashauri | 1,000,000,000 |
| 25. | Mfuko wa Jimbo | 36,325,000.00 |

| *Na* | Chanzo cha Mapato | Mapato 2022/2023 |
|---|---|---|
| 26. | Vyanzo Vingine (User Fee, iCHF na NHIF) | 305,624,987.68 |
| 27. | Global Fund | 86,826,000.00 |
| 28. | NTD | 21,164,208.00 |
| 29. | Mradi Mkakati wa Kuongeza Mapato, Soko la Kisasa (CBD). | 2,000,000,000 |
| **Jumla Ruzuku ya Maendeleo** | | **8,470,096,195.68** |
| **Jumla Miradi ya Maendeleo Ruzuku na Michango ya Jamii** | | **8,590,096,195.68** |
| **JUMLA KUU MIRADI YA MAENDELEO** | | **10,329,455,907.27** |

***Mheshimiwa Mwenyekiti***; Baada ya maelezo hayo naomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **45,832,490,885.50**. Naambatisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/2023 ili Kamati yako iweze kupitia na kupitisha. Aidha, Michanganuo ya Miradi ya Maendeleo na matumizi ya kawaida imeambatishwa katika ***kiambatisho namba 1 hadi 5***

Naomba kuwasilisha.

Eng. Mshamu A. Munde.

**MKURUGENZI**

**HALMASHAURI YA MJI KIBAHA**